MWITO PROG 1108 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE:ROMANS 6:23

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Nakukaribisha tena msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1108.Sina shaka kwamba Mungu amekulinda na hata kukufikisha siku ya leo ambapo tunakutana tena.Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na udhamini mkubwa wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake Harod Williams.Naamini umechukua kalamu na karatasi ili kunakili nasaha utakazozipata kwenye somo la leo,ambapo tumalizia malizia sura ya 6 tukitaraji kuikaribisha ille ya 7 ya kitabu cha Warumi.Unapojiandaa kwa kipindi cha leo Nakuchezea wimbo huu.. Karibuni waimbaji…..

Naam baada ya waimbaji wetu sasa hebu tuanze kutazama somo letu.Naomba tufungue aya ya 23 ya sura ya 6…… Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti;bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Bwana Kristo wetu.Naamini hakuna sehemu ilio na ukinzani kama ile inayoonekana kwenye aya hii.Kwa upande mmoja tunaona gharama kubwa ya dhambi.Twaona kuwa dhambi inahitaji adhabu kali.Na pia Mungu ni mwenye haki na mtakatifu kwa kutaka adhabu kama hiyo.Sababu yake ni kwamba dhambi hufanya mtu kuwa mtumwa.Dhambi huangamiza.Chochote kile kuhusu dhambi kinapingana na Mungu mwenye haki na mwenye upendo.Jinsi inavyojifunua sasa ni kwamba dhambi inapingana na haki ya Mungu na inataka adhabu kali.Ndiposa tunaona kwamba dhambi ambayo huwafanya watu kuwa watumwa inahitaji adhabu kali ;adhabu ya kifo.Na kifo ni lazima.Hapana njia ya binadamu kuepuka adhbu ya dhambi.Yesu kristo hata hivyo alilipa deni la dhambi kwa ajili ya Roho ya binadamu.Hapana matumaini hata katika muda wa miaka milioni 10 kulipa deni la dhambi za binadamu ,ambalo lililipwa na damu ya Yesu Kristo.Kwa hiyo hakuna chochote kinachoweza kufanywa na binadamu kulipa hilo deni.Kile ambacho tunahitaji kufanya ni kukubali kwamba hakuna chochote ambacho binadamu anweza kufanya kuhusu dhambi ya binadamu.Petero anatuambia kuwa alibeba dhmbi zetu katika mwili wake na kulipa kikamilifu deni la dambi.Aidha Isaya anatuambia kwenye sura ya 53 na aya y 11 kuwa….Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake na kuridhika kwa mmaarifa yake mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki,naye atayachukua maovu yao.Mungu ameridhika kabisa na kile Yesu alifanya na cho hote ambacho mwanadamu atajriu kufanya kitakuwa tu chukizo kwake.Rafiki yangu mshahara wa dhambi ni mauti au kifo.Lakini thawabu ya MUngu ni uzima wa milele kupitia mwanawe Yesu kristo,Bwan na mwokozi wetu.Ukijatibu kulilipa wewe kwa uwezo wako utakuwa unmchukiza Mungu ,wala hata huwezi kulilipia.Adhabu yadhambi ni ya kutisha.Lakini thawabu ya Mungu ni uima wa milele.Mpendwa huwezi kulipa gharama ya dhambi.Haya yote tumeelezewa kwenye sura za 3 na 4 za kitabu cha Warumi.Mtume Paulo alitueleza tofauti kuhusu kufanya kazi na kulipwa au kupokea mshahra au malipo.Huo ujira au mshahara hauwezi kuwa zawadi au thawabu,kwasababu ulifnya kazi kwa hiyo unastahili kulipwa wala huna haja ya kuomba msamaha kwa hilo.Yesu anapokupatia zawadi au thawabu unastahili kuipokea kwa shukrani.Lakini kinyume chake mpendwa,huwezi kufanya kazi na upokezwe zawadi.Utalipwa mshahara kwa sababu ulifany kazi.Zawadi hatuifanyii kazi hata kidoo.Zawadi na mshahara haviwezi kuendana .Vyanzo vyao ni tofauti.Kimoja kinatokana na kazi ,huku cha pili kikitokana na neema ya yule anayetoa hiyo zawadi.Kwa hivho kwa upande mmoja dhambi husababisha kifo,na upande wa pili Yesu Kristo hutupatia uhai.Thawabu ya Mungu au zawadi ya MUngu kwa binadamu ni

uzima wa milele.Neno la kigiri Ionion linatafsiriwa kuleta maana ya umilele.Aina ya uzima anaoutoa Mungu wetu muumba.Tfsiri nyingine inamaanisha uzima wa milele jinsi inavyosimuliwa kwenye kitabu cha Yohana 3:16.Uzima wa milele unazungumzia kuhusu muda.Ni kipindi kisichokuwa na mwisho.Neno hilo kikamilifu linamaanisha misha mazuri na yasio na mwisho.Mbona leo usifanye uamuzi wa kumpokea Kristo kuwa mwokozi wa maisha yako.Huo ndio uamuzi muhimu ambao unaweza kufanya maishani mwako.Nitafurahi sana ukichukua hatua na kufanya uamuzi huo muhimu kuhusu hatima ya maisha yako.Ungali una muda wa kufanya hivyo.Nakusihi ufanye amuzi,usije ukakumbwa na umauti kabla ya kuamua hatima yako.

Chukua fursa hii adhimu na utende unzlosthili kutenda ili usitahayari siku ya mwisho,kwamba wakati majina ya watakatifu yatakpoitwa ,lao halitakuwepo ambapo matokeo yke ni kutengwa na kurushwa huko Jehanami uipo na kusaga meno na vilio.

Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1108 Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari nitakayokupatia muda mfupi ujao. Tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Nitumie arafa yako kwa nambari hii -0721 970 520. Au 020 2679842 Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 15 sura ya 6 ya kitabu cha Warumi.Ni mimi ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mibaraka na neema tele zake zake Mungu.Bwana akubariki na udumu katika neema yake.Kwaheri.

……..XXXX……..

...